# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nianze kwa kumshukuru Allah (S.W), mwingi wa rehma na utukufu, kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kukutana tena leo hii katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar, kwa dhamira ya kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba, ambayo Waheshimiwa Wananchi wametutuma tuje kuyatekeleze hapa Barazani kwa niaba yao.

Aidha, nakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na wasaidizi wako kwa jitihada zenu na namna mnavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yetu kwamba, mtaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi katika kipindi hiki na kijacho, ili kuendeleza lengo na dhamira ya uwepo wa Baraza letu tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upekee kabisa na unyenyekevu mkubwa, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa busara na hekima zake kwa kuifikisha nchi yetu mpaka hapa tulipo, tukiwa katika hali ya amani na mshikamano, jambo ambalo tunajivunia. Tunazidi kumpongeza Mheshimiwa

Rais kutokana na jitihada, miongozo na maono yake hadi kuhakikisha Serikali inaendelea kuimarisha Sekta ya Ardhi na kuhakikisha matumizi ya rasilimali hii yanaleta tija na manufaa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

**Vile vile,** katika sekta ya Makaazi tunashuhudia kuongzeka kwa miradi mingi ya nyumba kwa ajili ya makaazi bora na biashara, ambako nako kunadhihirisha maono sahihi, kwa ajili ya watu sahihi na kwa wakati ulio sahihi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema na umri mrefu na azidi kumjalia mafanikio kwa yale yote aliyoyodhamiria.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliotuchagua. Ni wazi kwamba, wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani hio kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ile ile ya kutetea maslahi yao na Taifa kwa ujumla katika Baraza hili tukufu na kwengineko kote tunakowawakilisha.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe.Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote, na vile vile watendaji wa Wizara Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati tunapitia Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Lakini pia kwa namna ya kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kazi yao nzuri wakati wa kupitia Bajeti hii. Kwa hakika Wajumbe wa Kamati wameonesha umahiri, weledi na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha zinazoidhinisha na Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa lengo lakuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipeee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla | - | Mwenyekiti |
| 2. Mheshimiwa Aza Januar Joseph | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir | - | Mjumbe |
| 4. Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mohamed | - | Mjumbe |
| 5. Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir | - | Mjumbe |
| 6. Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame | - | Mjumbe |
| 7. Mheshimiwa Hassan Hamad Omar | - | Mjumbe |
| 8. Mheshimiwa Issa Haji Ussi | - | Mjumbe |
| 9. Mheshimiwa Simai Mohammed Said | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati hii inafanyakazi kwa kusaidiwa na Makatibu watatu ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu. Kwa hakika msaada wa makatibu hawa umekuwa chachu ya mafanikio makubwaya Kamati hii. Makatibu hao ni hawa wafuatao;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Himid Haji Choko | - | Katibu |
| 2. Ndg. Saad Othman Saad | - | Katibu |
| 3. Ndg. Salma Muhsin Haji | - | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka kwa  Wizara tunazo zisimamia,

hivyo katikakutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2024, Kamati yetu ilikaa na kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, na sasa kwa ruhusa yako, na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## UKUSANYAJI WA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,**

Tukisoma katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na Kiambatanisho nambari moja tunabaini kwamba, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha miezi tisa imekusanya asilimia **38% tu** kwa makadirio ya Mwaka. Hali hii inatia wasiwasi iwapo kwa robo nyengine iliyobakia Wizara inaweza kufika angalau nusu ya lengo lililo wekwa. Aidha, Kamati imebaini kuwa mapato yanayotokana na Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) ni asilimia **17%** tu ya makadirio. Kamati ilipohoji mapungufu haya majibu yalikua ni kwamba, changamoto iliyoelezwa mwaka jana bado inaendelea ambayo ni mkanganyiko wa ukusanyaji wa mapato hayo ambayo hukusanywa na taasisi nyengine pamoja na uhaba wa vitendea kazi vya ufuatiliaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaendelea kusisitiza kwa Wizara hii pamoja na Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa kukaa pamoja na kutafuta ufumbuzi wa suala hili na hatimae kuondokana na mkanganyiko unaendelea kuathiri utendaji kwa taasisi hizo.

## UPATIKANAJI WA FEDHA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu pia ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Shughuli za Kawaida, Huduma na Maendeleo kwa Wizara hii, ambapo Wizara imepatiwa asilimia **55%** ya Makadirio. Tunaiomba Serikali kuipatia Wizara hii fedha zote kama zilivyo ombwa na kwa wakati ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kukamilisha Malengo yake kama alivyojipangia.

Kwa upande mwengine, Kamati imeshtushwa na Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha ujao kwa Wizara hii kwani inaonekana kupanda kwa kiasi kikubwa kutoka Shilingi **Bilioni 53,062,900,000** hadi shilingi **Bilioni 345,485,900,000.**

Kamati ilipohoji juu ya ongezeko hili ilibaini kwamba, ongezeko hilo linatokana na uamuzi wa Serikali wa kutoa fedha zake za ndani katika kutekeleza Miradi ya Wizara hiyo ikiwemo Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Taarifa za Ardhi (LARIS) na Ujenzi wa Nyumba za Makaazi Bora, Biashara na Maendeleo.

### Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Wizara kupitia Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu, Wizara imeripoti kua, Mahakama ya Ardhi imepokea mashauri mapya **170** ambayo yamefunguliwa Mahakamani Unguja na Pemba. Tarakimu hizi zinaonesha kuongezeka kutoka mashauri **135** mwaka jana katika kipindi kama hiki. Hali hii pia inaonesha kuendelea kuongezea wimbi la migogoro ya Ardhi katika jamii yetu.

Utafiti wa Kamati umebaini kuwa Migogoro mingi ya Ardhi inatokana na mipaka, eneo moja kuuziwa au kumilikishwa mtu zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja, uvamizi wa maeneo ya wazi au yaliyoachwa kuendelezwa kwa muda mrefu, kuongezeka kwa thamani ya ardhi yenyewe, na kukua kwa Miji na Vijiji.

**Hivyo, Mheshimiwa Spika,** tunaiomba Wizara kuongeza jitihada za kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya mashauri yote yanayohusiana na Migogoro ya ardhi ambayo yako mahakamani na migogogoro mingine ya ardhi kwa kuzingatia misingi ya haki, weledi na uadilifu bila ya kudhulumu upande wowote.

**Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,**

Kuhusiana na Utekelezaji wa Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ardhi ambayo inatekelezwa na Mthamini Mkuu wa Serikali tumebaini kuwa, bado Afisi hiyo inaendelea na Marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu pamoja na Bodi ya Usajili wa Wathamini Zanzibar. Kamati inamatumaini kwamba, kukamilika wa Sheria hiyo kutasaidia kuweka usimamizi mzuri wa kazi za uthamini hapa nchini, badala ya mtindo wa hivi sasa ambapo tunashuhudia malalamiko mengi ya wananchi ambao hawaridhishwi na kazi za uthamini kwa sasa, na hivyo kuwa na malalamiko mengi yasiyokuwa ya lazima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imekuwa ikipokea malalamiko kadhaa kutoka kwa wananchi hasa waliopisha miradi katika sekta za Mawasiliano na Usafirishaji, pamoja na Miundombinu ya Maji na Umeme ambao hawakuridhika na Fidia waliyopewa kwa kuhisi kuwa wamedhulumiwa kutokana na madai ya kutotendewa uadilifu wakati wa uthamini, ambapo kwa upande mwengine anaelipa fidia nae anahisi anatoa kingi kulingana na thamani ya mali inayofidiwa. Kamati inaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kukamilisha michakato iliyobaki, ili kukamilisha sheria hiyo kwa haraka na kuondosha madhaifu yanayojitokeza hivi sasa.

**Upangaji na Usimamizi wa Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**,

Kamati inaipongeza Wizara kupitia Utekelezaji wa Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ardhi, inayotekelezwa na Kamisheni ya Ardhi ambapo tunashuhudia kukamilika kwa zoezi la upangaji wa Mji wa Mahonda na kuendelea na Mji wa Gamba kwa Upande wa

Unguja.

**Vilevile,** tumeridhika na maendeleo ya upangaji katika maeneo ya Kojani na Mvumoni kwa Pemba. Kamati inaendelea kuhimiza kasi ya utedaji, ili kukamilisha upangaji wa maeneo hayo pamoja na kufikiria kupanga maeneo mapya ili kwenda sambamba na kasi ya maendeleo hapa nchini.

Wakati huohuo, tunaishauri Idara ya Mipango Miji na Vijiji ya Kamisheni ya Ardhi kuwa karibu zaidi na taasisi nyengine zinazohusika na uwekaji wa Miundombini ya huduma za kijamii ikiwemo Ujenzi wa Barabara,Umeme na Maji safi na Serikali za Mitaa ili kuwa na mipango ya pamoja na kuepusha usumbufu na uharibifu unaojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

**Shirika la Nyumba**

**Mheshimiwa Spika,**

Nimalizie uchambuzi wa bajeti kwa Wizara hii kwa kuangalia Taasisi yetu ya Shirika la Nyumba. Kamati inaridhishwa na kuunga mkono juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi hadi kufikia maendeleo yaliyopo katika sekta ya Nyumba na Makaazi kama utekelezaji wa Wizara unavyoonekana kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Aidha, Kamati inawaomba waheshimiwa Wajumbe wote kuunga mkono mipango na malengo ya Shirika la Nyumba hapo mwakani kwa kuwaidhinishia fedha zote walizoomba ili kutekeleza kwa ufanisi miradi ya nyumba bora za makaazi na biashara pamoja na kuzifanyia matengenezo nyumba zake zilizochakaa ambapo miradi yote hiyo inalenga kuimarisha makaazi ya wananchi pamoja na kuboresha mandhari ya maeneo yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na juhudi hizo za Serikali ambazo tunazithamani kwa kiasi kikubwa, bado tunaiomba serikali yetu sikivu kuangalia upya dhana ya nyumba za **“Bei nafuu”** ili

wananchi wa vipato tofauti waweze kumudu gharama za kununua au kukodi nyumba hizo ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na matunda ya serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kumaliza uchambuzi wa Kamati, kwa mara nyengine tena, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba hii kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifuatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza.

Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza Mipango aliyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,** naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………………………………..

**(Mhe: Yahya Rashid Abdulla).**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**